

BARAZA LA HABARI TANZANIA



S.L.P 10160, Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255-22-2775728/2771947
0732998310

Simu ya mkononi: +255-784-314880
Nukushi: +255-22-2700370,0732991521
Barua pepe: media@mct.or.tz
Tovuti: <http://www.mct.or.tz>
Zanzibar Office: P.O.Box 3490,
Tel/Fax: +255-24-2239728
Email: mctz@mct.or.tz

P.O.Box 10160, Dar es Salaam, Tanzania
Tel: +255-22-2775728/2771947/
0732998310

Mob: +255-784-314880
Fax: +255-22-2700370,0732991521
Email: media@mct.or.tz
Website: <http://www.mct.or.tz>

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari Tanzania kutolewa Mei 3, 2011

Kamati ya Maandalizi ya Tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari Tanzania (EJAT) imeandaa usiku maalum ambapo kutakuwa na hafla ya kuwazawadia waandishi wa habari ambao walifanya vizuri katika makundi mabalimbali ya uandishi kwa mwaka 2010. Hafla hiyo itafanyika Mei 3, 2011 katika ukumbi wa Mlimani City, jijini Dar es Salaam.

Kamati ya Maandalizi inaongozwa na Baraza la Habari Tanzania (MCT) na inajumuisha Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake (TAMWA), Chama cha Waandishi wa Habari za Michezo (TASWA), HakiElimu, Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira Tanzania (JET), Chama cha Waandishi Walio katika Mapambano Dhidi ya Ukimwi (AJAAT), Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), Taasisi ya Uandishi wa Habari Kusini mwa Afrika- Tawi la Tanzania (MISA-TAN), Chuo Kikuu cha Johns Hopkins na Chama cha Wamiliki wa Vyombo vya Habari Tanzania (MOAT).

Hafla hiyo itatanguliwa na shughuli nyingi ikiwa ni pamoja nah ii ya leo ya kuzindua rasmi Tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari . Kwa hivyo basi Kamati inawaomba waandishi wa habari ambao wanataka kushiriki katika mashindano haya ya tuzo kutuma kazi zao ambazo zilichapishwa gazetini au kutangazwa kwenye radio au televisheni kuanzia Januari 1, 2010 mpaka Desemba 31, 2010. Fomu za ushiriki zinapatikana MCT, kwenye tovuti ya MCT na zitasambazwa katika klabu za waandishi wa habari na katika ofisi za vyombo vyote vya habari.

Kamati ya Maandalizi imeteua majaji ambao ni watu waadilifu, wanaoheshimika katia jamii na ambao wana uzoefu katika masuala ya habari. Mchakato wa kupata mshindi katika tuzo hizi utafuata vigezo maalum vya kitaaluma kwa habari zilizochapishwa magazetini au kutangazwa katika radio na televisheni. Mahsusi kabisa, majaji wataangalia kama habari inayoshindanishwa inasaidia kutoa maarifa mapya kuhusu suala muhimu katika jamii, upekee wa kazi ya mwandishi; ubunifu , utafiti na ubora wa namna kazi ya mwandishi ilivyowasilishwa; umahiri katika lugha; kiwango cha kufuata maadili ya kitaaluma ikiwa ni pamoja na kusema ukweli, usahihi, ustaarabu na kuweka urari katika habari.


*For a strong and ethical media that contributes
towards a more democratic and just society*

Katika tuzo za mwaka huu, waandishi watatakiwa kushindanisha kazi zao katika makundi 16 yafuatayo:

1. Tuzo ya Uandishi wa habari za Utawala Bora, upande wa magazeti, radio na televisheni;
2. Tuzo ya Uandishi wa habari za Jinsia upande wa magazeti, radio na televisheni;
3. Tuzo ya Uandishi wa habari za Uchumi na Biashara, upande wa magazeti, radio na televisheni;
4. Tuzo ya Uandishi wa habari za Michezo na Utamaduni, upande wa magazeti, radio na televisheni;
5. Tuzo ya Uandishi wa habari za Mazingira, upande wa magazeti, radio na televisheni;
6. Tuzo ya Uandishi wa habari za Afya, upande wa magazeti, radio na televisheni;
7. Tuzo ya Uandishi wa habari za Virusi vya Ukimwi na Ukimwi, upande wa magazeti, radio na televisheni;
8. Tuzo ya Uandishi wa habari za Malaria, upande wa magazeti, radio na televisheni;
9. Tuzo ya Uandishi wa habari za Watoto, upande wa magazeti, radio na televisheni
10. Tuzo ya Uandishi wa habari za Elimu, upande wa magazeti, radio na televisheni;
11. Tuzo ya Uandishi wa habari kuhusu Kazi na Mahusiano kazini, kwa upande wa magazeti, radio na televisheni;
12. Tuzo ya Mpiga Picha Bora
13. Tuzo ya Mchoraji Bora wa Vibonzo;
14. Tuzo ya Uandishi wa habari za Mawasiliano, upande wa magazeti, radio na televisheni;
15. Tuzo ya habari za Sayansi na Teknolojia, upande wa magazeti, radio na televisheni;
16. Tuzo ya Uandishi wa habari za Watu Wenye Ulemavavu, upande wa magazeti, radio na televisheni;

Kutakuwa na Kundi la Wazi la ambalo ni kwa ajili ya waandishi ambao kazi zao hazikuweza kuingia katika makundi yaliyotajwa hapo juu.

Washindi wa kila kundi watazawadiwa vyeti, vikombe na zawadi ambazo zitatangazwa baadaye. Pia kutakuwa na mshindi wa jumla ambaye atafaidika kwa kugharamiwa masomo katika fani yoyote inayohusiana na habari ili mradi gharama yake isizidi Dola za Kimarekani 4,000.


Kajubi D. Mukajanga

Katibu Mtendaji

Machi 10, 2011